# Uainishaji wa maeneo ya uchimbaji mdogo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania

*Utafiti juu ya uasili, wigo na athari zake*

**Muhtasari**



IPIS

*International Peace Information Service vzw*

# UHARIRI

**Uainishaji wa maeneo ya uchimbaji mdogo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania: Utafiti juu ya uasili, wigo na athari zake – Muhtasari**

Antwerp/Mwanza, Januari 2018

**Picha ya mbele**: Eneo la mgodi wilaya ya Serengeti, Mkoa wa Mara (2017 – Picha na: IPIS)

**Mwandishi**: Hans Merket

**Uratibu wa tafiti na miradi Tanzania**: Elard Mawala

**Ramani, hifadhidata na michoro:** Manuel Claeys Bouuaert, Emily Doerner & Stef Verheijen

**Uhariri**: Ken Matthysen

**Shirika la IPIS** ni taasisi huru inayojihusisha na utafiti inayotoa taarifa maalum, uchambuzi na utoaji mafunzo kwa wadau wakubwa wanaotaka kuona ndoto inatimia juu ya amani ya kudumu, maendeleo endelevu na haki za binadamu zinazingatiwa.

Ripoti hii, hifadhidata ya wazi, na ramani ya tovuti jumuishi (http://ipisresearch.be/mapping/webmapping/tza/v1) inayoambatana nayo ni sehemu ya mradi wa 'Uanishaji wa athari za migodi midogo na mikubwa kijamii, kiuchumi na kwenye haki za binadamu kaskazini magharibi mwa Tanzania'. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji kama sehemu ya programu ya Haki za Binadamu na matumizi ya teknolojia ya kidijitali.

With the support of
THE BELGIAN
DEVELOPMENT COOPERATION .be

D/2019/4320/03

# MUHTASARI[1]

Utajiri mkubwa wa madini nchini Tanzania unatoa fursa muhimu ya maisha na biashara kwa wachimbaji wengi wadogo wa madini. Katika muongo uliopita, Tanzania ilipiga hatua kubwa sana katika kutengeneza nyaraka za sera na sheria zenye kusimamia uchimbaji mdogo. Hata hivyo, utekelezaji na utii wa sheria ndio vimebaki changamoto kutokana na ugumu katika kukabiliana na sekta hii mtambuka.

Picha kuu ya uchimbaji mdogo Tanzania ni moja ya kazi mbovu zenye athari hasi kwa upande wa afya, usalama na mazingira. Fikra hii ambayo bado ina utata inasababishwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa uthibitisho kwenye sekta. Wakati tafiti nyingi na ripoti hazijaonesha maeneo mahusisi ya kijiografia au kimaudhui juu ya uchimbaji mdogo Tanzania, hadi sasa hakuna takwimu nyoofu, za kueleweka na zenye uwakilishi mzuri juu ya uasili, mapana na athari zake kwenye hali ya kijamii, kiuchumi na haki za binadamu nchini. Takwimu nyingi zinaonekana ni za kupikwa tu na siyo zilizotokana na chambuzi za kina. Hatima ya ukosekanaji wa taarifa hizi ni kikwazo cha maendeleo ya sera thabiti katika kusimamia sekta ya uchimbaji mdogo na mchango wake kwa maendeleo.

Lengo la ripoti hii, na ramani ya tovuti shirikishi (http://ipisresearch.be/mapping/webmapping/tza/v1) pamoja na hifadhidata ya wazi (http://ipisresearch.be/home/conflict-mapping/maps/open-data/) ni kutoa mchango katika kuleta uelewa bora na wenye mizania zaidi juu ya sekta na athari zake. Kama hatua ya kwanza katika ukusanyaji wa data nyoofu, uhifadhi na uchambuzi wa data juu ya uchimbaji mdogo Tanzania, IPIS ilikusanya taarifa za tafiti kwa kutumia simu za kiganjani kwenye mikoa minne kaskazini magharibi mwa Tanzania, ambayo ni Geita, Shinyanga, Mara na Kigoma. **Maeneo 447 ya uchimbaji na uchakataji wa madini** yaliainishwa na kufanyiwa utafiti. Kati ya hayo, 337 ni ya dhahabu, 84 ya chokaa, 11 ya chumvi, 5 ya almasi, na 10 ni ya aina nyingine za madini ikiwa ni pamoja na shaba, madini ya kioo, galena na maginetiti.




1 Toleo kamili la ripoti inapatikana kwa Kiingereza hapa: http://ipisresearch.be/publication/mapping-artisanal-small-scale-mining-northwest-tanzania/.

Kuna **wachimbaji** wapatao kati ya 75,600 na 92,400 waliokuwa wanajihusisha moja kwa moja kwenye uchimbaji na uchakataji wa madini kwenye mikoa hii minne kipindi cha masika, wakati wa ukusanyaji wa taarifa hizi za utafiti. Kati yao 98% wanafanya kazi kwenye uchimbaji na uchakataji wa dhahabu, na hii ndio kiini cha ripoti hii. Kipindi cha kiangazi, mazingira ya kazi huwa mazuri zaidi, na idadi ya wafanyakazi inakadiriwa kupanda hadi kati ya 99,300 na 121,400. Ukijumlisha na huduma nyingine ndogo ndogo kama usafiri, ujenzi, biashara, migahawa, na nyumba za kulala wageni, tunakisia idadi ya watu wanaojihusisha kwa njia moja au nyingine kwenye migodi midogo inafika kati ya 302,400 na 485,600 kwenye mikoa hii minne.






Wachimbaji na wachakataji ni kundi la watu wanaohamahama. Hasa kwenye migodi ya dhahabu, kuna uvamizi sana kaskazini magharibi mwa Tanzania ambapo maelfu ya wafanyakazi huingia na kutoka kwa miezi tu. Mfanyakazi mmoja kati ya watatu huja akitokea mkoa mwingine, na wengine wengi husafiri kwenye mikoa hii mikubwa wakisaka fursa za ajira. Mara kadhaa migodini hakuna miundombinu ya kutosha kukabiliana na umati huu wa wafanyakazi. Zaidi ya nusu ya wafanyakazi hufanya kazi kwenye migodi yenye kambi za muda ambamo familia 1 kati ya 4 huishi na kulala. Ni wazi **hamahama** hii inaleta shida kwenye kuwekeana taratibu na urasimishaji, ikiwa ni 77% ya wachimbaji na wachakataji wanafanya kazi kwenye maeneo ya machimbo ambayo bado hayana leseni.



*Kambi ya Wachimabaji Chokaa Makere, Kigoma ( 2018 – Picha: IPIS)*

Ili kukabiliana na hamahama hii na kueneza uwekezaji na kuepuka majanga, miundo yenye sura kadhaa imeshaundwa, ikiwa na milolongo sahihi ya kimajukumu na mifumo ili kuwagawa wafanyakazi na kugawana wanachozalisha. Zaidi ya hayo, zaidi ya nusu ya wafanyakazi wana nguvu ya pamoja kwenye maeneo yao na wale wenye leseni wanawakilishwa kwa kupitia vyama vya wachimbaji ngazi ya mkoa. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa za kimuundo, hasa kutokana na uongozi mbovu, majukumu kutosimamiwa vizuri, kutokuwa na usawa wa kijinsia na kutopata fedha. Hili la mwisho linafifisha pia upigaji hatua wa sekta, ambapo 55% ya migodi bado inatumia nyenzo za mikono, kama vile mabeleshi, masururu na nyundo. Sekta ya uchakataji wa madini yenyewe inakwenda kwa kasi zaidi, ambapo ni chini ya 20% tu ndio inatumia nyenzo duni. Pasipo mipango ya kurasimisha kuwezeshana kupata fedha, mitaji mikubwa kwenye sekta ya uchimbaji mdogo itapitia kwenye mitandao ya wafanyabiashara wa dhahabu ambayo ndio yenye kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli ambapo mwishowe ndio wanabaki kuhodhi (sehemu ya) uzalishaji. Hii inasababisha wachimbaji waangukie kwenye dimbwi la madeni, kushindwa kuendesha shughuli zao kwa njia halali na kutoelewana.

> ***"Benki zetu hazitutambui. Wakati wanatoa mikopo ya kutosha kwa wakulima, hawaoni upande wa migodi midogo na hivyo kushindwa kujihusisha nasi au wanafanya tu kwa masharti magumu sana. Tunaiomba serikali iweke masharti nafuu ya mikopo."***
> (mmiliki wa leseni Nyakagwe, mkoa wa Geita)

Kupata mikataba na mishahara ni nadra. Wafanyakazi kwa ngazi tofauti tofauti kwenye uchimbaji mdogo wanapata **kipato** chao kwa kupitia mipango holela jumuishi ya uzalishaji au kwa kujipatia malipo kutokana na walichozalisha. Hii inasababisha tofauti kubwa sana baina ya madini lakini pia kati ya uchimbaji na uchakataji wa madini. Uchimbaji wa dhahabu unalipa zaidi, ambapo mfanyakazi hupata USD 90 hadi USD 110 kwa mwezi. Wachakataji wa dhahabu hupata wastani wa chini ya 10%. Uzalishaji wa chumvi ndio uko chini kabisa katika ulipaji, sababu mojawapo ikiwa ni kwamba uzalishaji huwa unasimama kipindi cha mvua, na hivyo kwa wastani mfanyakazi hupata USD 25 hadi USD 31 kwa mwezi.

> ***"wachimbaji wadogo ni kama mbwa wawindao, wakishamkamata mnyama mwindaji huamua nini awape hao mbwa"*** *(*mchimbaji huko Nyakagwe, Geita*)*

**Wanawake** wananufaika kwa kiasi kidogo kutokana na utajiri huu wa madini ukilinganisha na wanaume. Wao ni 20% tu ya wafanyakazi wote na mara nyingi hubaki kwenye nafasi za chini. Mara nyingi huwa kwenye shughuli za uchakataji wa madini zaidi kwa mfano kupasuapasua mawe na kutenganisha madini na kokoto, ambazo huingiza kipato cha hadi kufikia 66% chini ya kile wachimbaji wanapata. Maeneo ya uchimbaji mdogo kwa kiasi kikubwa ni ya kimfumo dume maana wanaume wanalinda sana nafasi zao. Maeneo ya uchimbaji mdogo hayajamthamini mwanamke, kwa mfano, 11% tu ya maeneo haya yametenga huduma za vyoo kwa ajili ya wanawake. Cha kushangaza zaidi, uzalishaji kwenye maeneo mengi usingewezekana bila wanawake, ambao hutoa mchango mkubwa kwenye huduma ndogo ndogo kama vile chakula, vinywaji, ufundi na usafirishaji.



*Wanawake wakiponda mawe (Shinyanga, 2017 – Picha : IPIS)*

**Watoto** wengi huishi migodini na sehemu za uchakataji wa madini na kuzunguka hayo maeneo. Kwa miaka ya hivi karibuni kuna juhudi nyingi zimefanywa kuwazuia wasijihusishe na shughuli za uchimbaji. Hawa wanaonekana kufanikiwa, kama ambavyo Shirika la IPIS liliwabaini watoto wanne wa chini ya umri wa miaka 15 waliokuwa wanajihusisha na shughuli za migodini. Hata hivyo, kujihusisha kwao na uchakataji wa madini bado ni kukubwa, kwani 15% ya maeneo ya uchakataji wa madini bado yanawatumia watoto. Nusu ya sehemu hizi za uchakataji wa madini zina ajira kwa watoto, ambao taarifa zinaonesha wanafanya kazi wakati vipindi mashuleni vinaendelea.



*Mtoto akichenjua dhahabu (Mara, 2018 – Picha: IPIS)*

**Afya na usalama** ni muhimu kuzingatiwa kwenye maeneo mengi ya migodi midogo. 30% ya wafanyakazi hawana vyoo safi kwenye maeneo yao ya kazi, na vilivyopo vina hali mbaya au havitoshi. Ukiunganisha na uhaba wa maji safi na salama ya kunywa, zagaazagaa ya vumbi na kelele, hapo panakuwa mazalia ya maambukizi na magonjwa mengi. Kwa kuongezea, zaidi ya 17% za maeneo haya yalikumbwa na ajali mwaka mmoja kabla ya utafiti huu wa IPIS. Ajali hizi ziliwajeruhi angalau wafanyakazi 175 na kuua 90. Mashimo kuporomoka vinahusika kwa kama nusu ya majeruhi na theluthi moja ya vifo. Sababu nyingine kuu ni wafanyakazi kuanguka au kuteleza wakati wanaingia au kutoka kwenye mashimo ya migodi na mitambo kutofanya kazi. Suala la usalama halizingatiwi, uchimbaji unatumia mbinu duni na matumizi ya vifaa vya kujikinga na ajali ni mdogo. Helmeti, kwa mfano, zinavaliwa na 16% tu ya migodi yote, na hapo ni wachimbaji wachache tu ndio wanachaguliwa kuzivaa.



*Mchimbaji akishuka kwenye shimo "duara" (Geita, 2017 – Picha: IPIS)*







Matumizi ya zebaki, kemikali ambayo ina sumu ya hali ya juu,inayotumika kwenye uchakataji wa dhahabu nayo ni muhimu sana kuangaliwa kwa jicho la kipekee kwenye suala la afya. Matumizi yake yalionekana kwenye maeneo mengi ya uchakataji wa dhahabu. Pamoja na uhamasishaji na kampeni za mafunzo juu ya kuwa makini katika kutumia zebaki, vitendo vitatu kati ya vine, ambavyo vimetajwa kwenye Mkataba wa Minamata wa Matumizi ya Zebaki wa mwaka 2017, vinatendwa sana maeneo hayo. Kwanza, ni mara chache kutumia mitambo ya kuyeyushia na kuchujia dhahabu. Mchanganyiko wa dhahabu na zebaki mara nyingi unaungua hewani, na hivyo kusababisha mvuke wenye sumu kali hewani. Pili, 71% ya maeneo yanayotumia zebaki yako karibu na makazi ya watu, ambamo watoto huishi na kucheza, wanawake wanaandalia vyakula, na kaya zinamojihusisha na kilimo cha kujikimu.

Mwisho, uchenjuaji kwa kutumia kemikali ya sayanaidi ni biashara inayokua kwa kasi kwenye maeneo haya. Vinu hivi vina ufanisi Zaidi katika kuchakata dhahabu na kwa hiyo kuna uwezekano wa kupungua kiasi cha zebaki kinachotumika katika uchimbaji mdogo.Hata hivyo wakati wa kukusanya taarifa hizi. Vinu vya uchenjuaji vilikua vikinunua makinikia kutoka kwenye migodi midogo na kuichakata bila kutoa mabaki ya zebaki. Hili ni tatizo kwa kuwa mgusano na kemikali ya sayanaidi husababisha zebaki kuwa hatari zaidi kwa kuwa huharakisha kemikali ya zebaki kuingia kwenye maji, udongo na hewa.



*Caption: Mchenjuaji akiunganisha ("akikamata") dhahabu kwa kutumia zebaki (Mara, 2018 – Picha: IPIS)*




Uchimbaji mdogo huathiri pia mazingira kaskazini magharibi mwa Tanzania kupitia uchafuzi wa vyanzo vya maji, ukataji miti pamoja na uharibifu wa ardhi. Kwa kuwa wafanyakazi wawili kati ya watatu wanafanya kazi karibu na makazi ya watu, usumbufu huu unaziathiri **jamii husika**. Wakati migongano ni kawaida kuwepo, ugomvi wa hali ya juu ni kama haupo maana wanaoathirika ni 2% tu ya wafanyakazi wote. Kuna sababu kadhaa katika hili. Kitu kimoja cha kushika ni kwamba uchimbaji ni jadi ya jamii nyingi. Wakazi wengi hujihusisha kwa njia moja au nyingine kwenye sekta hii kwa ajili ya kujipatia kipato. Zaidi ya nusu ya maeneo yote ya uchimbaji na uchakataji wa madini yana uwajibikaji wa pamoja ambao unachangia kwenye afya, elimu, barabara na miundo mbinu ya vijiji jirani. Zaidi ya hayo, wadau wengi, ikiwa ni pamoja na vyama vya wachimbaji wa madini ngazi ya mkoa, mamlaka za migodi na vijiji wana nafasi kubwa sana katika kuzuia na kusuluhisha migogoro.



*“Ziara za serikali ni nzuri kwetu kwani zinatupa kujua yale ambayo hatukujua mwanzoni, au kutukumbusha maonyo ambayo tulishasahau” (mmiliki wa kitengo cha uchakataji wa dhahabu Katente, Geita)*

Kwa kuzingatia mambo kadhaa hapo juu, ni wazi kwamba kuna kazi kabambe ya kufanya ili kuhakikisha mfumo wa sheria ya madini Tanzania unafuatwa. Kwa uchache taasisi 10 za **serikali** zinahusika na **usimamizi**, na kwa pamoja wanatembelea 94% ya maeneo ya uchimbaji na uchakataji wa madini. Wanafanya ukaguzi kadhaa, ikiwa ni pamoja na usalama, mazingira, na afya, wanakusanya kodi, mirabaha na ada, wanatoa mafunzo na misaada, wanakusanya taarifa(data), wanahakikisha usalama wa afya na sheria vinafuatwa, na kutatua migogoro. Hata hivyo, ushirikiano na kupeana taarifa baina ya watumishi wa serikali kwa sasa si mzuri kwa sababu ya kukosekana kwa uratibu mzuri kutoka serikali kuu. Matokeo yake, maeneo mengi yanatembelewa mara chache, kukiwa na jambo moja mahususi, au bila kujua nini au kaguzi zilizofanyika kipindi cha nyuma. Kuandaa utaratibu na mfumo wa uratibu wenye mgawanyo bainishi wa madaraka pamoja na njia za mawasiliano kunaweza kukaongeza ziara zaidi, ufanisi, maboresho na kufuatilia kwenye tija katika usimamizi wa sasa.